

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUITWA KWENYE  
USAILI (ORAL INTERVIEW)**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) anapenda kuutangazia umma kwamba usaili wa ana kwa ana (Oral Interview) kwa walioomba nafasi za kazi TAKUKURU utafanyika Jijini Dodoma kuanzia tarehe 27 Machi, 2023.

**Mambo muhimu ya Kuzingatia**

1. Tarehe ya usaili ni kuanzia tarehe 27 Machi, 2023;
2. Usaili utakuwa unaanza saa 2:00 asubuhi kila siku;
3. Kila mtu aliyeitwa kwenye usaili anatakiwa kufika kwenye usaili kwa siku na muda aliopangiwa akiwa na nyaraka zifuatazo:-
  - 3.1 Nakala halisi za vyeti vya masomo (Taaluma na kozi mbalimbali)
  - 3.2 Picha tatu "Passport Size"
  - 3.3 Nakala halisi ya cheti cha kuzaliwa
  - 3.4 Namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kadi
  - 3.5 Anuani, namba ya simu na picha za wadhamini wawili;
4. Kuwasilisha nyaraka za kughushi ni kosa la jinai;
5. Kila mtu atakayefika kwenye usaili huu anapaswa kujigharamia;
6. Majina ya watu wote walioitwa kwenye usaili pamoja na eneo la kufanyia usaili yanapatikana kwenye wavuti ya TAKUKURU [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)
7. Watakaofaulu kwenye usaili wa mahojiano ya ana kwa ana ndio watakaojulishwa.

Imetolewa na

Mkurugenzi Mkuu,  
Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa,  
Mtaa wa Jamhuri,  
S.L.P. 1291,  
**41101 DODOMA.**